

Tunalaani Uvamizi wa Majeshi ya Urusi dhidi ya Ukraini

Tunalaani uvamizi wa majeshi ya Urusi dhidi ya Ukraini na kudai kwamba serikali ya Urusi isitishe mashambulizi dhidi ya nchi hiyo na kuondoa majeshi yake kutoka nchini Ukraine mara moja na bila masharti yoyote.

Kujieleza kwa maneno kumekuwa vigumu siku hizi, kutokana na ukweli kwamba maneno yanaweza kufasiliwa kinyume na maana iliyokusudiwa. Hata hivyo, sisi kama watafiti wa mambo yanayohusu lugha na jamii, tunaamini kwamba suluhisho ni maneno na si silaha ("Kalamu ina nguvu kuliko upanga").

Kutokana na uzoefu wa kihistoria ulimwenguni mifanano yetu na tofauti zetu za lugha na utamaduni zimekuwa zikitumiwa katika vita mbalimbali. Hata hivyo, tulilitambua hili na tumekuwa tukijitahidi kuchukua hatua zinazotuelekeza kupata masuluhisho ya mambo ya lugha na utamaduni bila kutumia silaha au nguvu. Uvamizi wa majeshi ya Urusi dhidi ya Ukraini mara hii ni jambo linalokinzana na jitihada zetu.

Tunapeleka rambirambi za dhati kwa watu waliopoteza maisha katika mashambulizi haya na kutoa pole kwa wote walioathirika na mashambulizi hayo. Aidha, tunaungana na wote wanaopaza sauti kupinga uvamizi huu wa kijeshi. Pamoja na hayo, tunapinga udhalilishaji na kashfa zinazoelekezwa kwa watu wa Urusi.

Matatizo yote yanatakiwa kusuluuhishwa kupitia majadiliano na kwa njia ya amani.

Membu wa Chama cha Watafiti wa jamii wingi-lugha,
Watafiti wa Mambo ya wingi-lugha,
Wahariri wa Jarida la "Lugha na Jamii" (Kotoba to Shakai)

Machi 4, 2022